***Fasiri ya Jumla ya Taaluma ya Stadihaki Jamii***

Stadihaki jamii ni utendaji halisi katika weledi na nidhamu ya taaluma inayochochea mabadiliko na maendelelo ya kijamii, mshikamano wa kijamii, na uwezeshaji na ukombozi wa watu. Kanuni za haki ya jamii, haki za binadamu, uwajibikaji wa pamoja na kuheshimu tofauti mbalimbali miongoni mwetu ni muhimu sana katika stadihaki jamii. Kwa mujibu wa nadharia za huduma jamii, sayansi za jamii, elimu jamii,utu na maarifa ya asili ya wazawa, stadihaki jamii huhusisha watu na miundo kushughulikia ukizani katika maisha na kujenga ustawi.

Fasiri hiyo hapo juu inaweza kutumika katika ngazi za kitaifa na/au kimkoa/kikanda.

## UFAFANUZI

Ufafanuzi hutumika kueleza kwa kina dhana za msingi zilizotumika katika fasiri kwa kuhusisha na mamlaka ya msingi, kanuni, maarifa na utendaji wa taaluma ya stadihaki jamii.

## MAMLAKA YA MSINGI

Mamlaka ya msingi ya taaluma ya stadihaki jamii hujumuisha kuchochea mabadiliko ya kijamii, maendeleo ya kijamii, mshikamano wa kijamii na uwezeshaji na ukombozi wa watu.

Stadihaki jamii ni utendaji halisi katika taaluma unaotambua kwamba sababu au vipengele changamani vya kihistoria, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni, kimahali, kisiasa na kibinafsi hutumika kama fursa na/au vikwazo kwa ustawi na maendeleo ya binadamu. Vikwazo vya kimuundo huchangia kuendelea kwa kukosekana usawa, ubaguzi, unyonyaji na ukandamizaji. Maendeleo ya utambuzi makini kwa kuangalia vyanzo vya kimuundo vya unyanyasaji na/au manufaa au faida, kwa msingi wa vigezo kama vile rangi, tabaka, lugha, dini, jinsia, ulemavu, utamaduni na mwelekeo wa kijinsia, na kuendeleza hatua za kimkakati katika kukabiliana na vikwazo binafsi na vya kimuundo ni muhimu sana katika jitihada za kiukombozi ambapo malengo ni uwezeshaji na ukombozi wa watu. Katika kushikamana na wale walioachwa kando, taaluma hii inajaribu kupunguza umaskini, kuwakomboa walio katika mazingira magumu na wanaonyanyaswa na kuhamasisha ushirikishwaji na mshikamano wa kijamii.

Mamlaka ya mabadiliko ya kijamii huegemea kwenye nguzo kwamba mwingiliano wa stadihaki jamii hutokea pale ambapo hali iliyopo, iwe katika ngazi ya mtu binafsi, familia, kikundi kidogo, jumuiya au jamii, inaonekana kuwa yenye kuhitaji mabadiliko na maendeleo. Msukumo hutokana na haja ya kukosoa na kubadilisha hali za kimuundo zinazochangia kusahaulika, kutengwa na kunyanyaswa kijamii. Mipango ya mabadiliko ya kijamii inatambua nafasi ya binadamu kama wakala katika kuendeleza haki za binadamu, kiuchumi, kimazingira na usawa wa kijamii. Taaluma hii imejizatiti kisawasawa kuendeleza utulivu wa kijamii, ili kuhakikisha kwamba utulivu huo hautumiwi kukisahau, kukitenga au kukinyanyasa kikundi chochote cha watu.

Maendeleo ya kijamii hutumiwa kumaanisha mikakati ya kuchochea matokeo yanayotarajiwa na mfumo wa sera, ambapo hili la pili hujitokeza sambamba na miundo muhimu zaidi ya kitaasisi. Hayo huegemea katika miundo ya jumla ya kibiolojia, kisaikolojia na kijami, tathmini na ushauri wa kiimani/kiroho ambao unadhihirisha migawanyiko kadha ikihusisha ngazi mbalimbali za kimfumo na zile za kisekta, pamoja na uhusishwaji wa taaluma mbalimbali kwa lengo la kuleta maendeleo endelevu. Stadihaki jamii pia huweka vipaumbele vya maendeleo ya kijamii, kiutamaduni, na kiuchumi, na wala haifuati mtazamo wa kilimwengu kwamba maendeleo ya kiuchumi ndio msingi wa maendeleo ya kijamii.

**KANUNI**

Kanuni muhimu ya Stadihaki jamii ni kuheshimu thamani na utu wa binadamu, kutodhuru wengine, kuheshimu tofauti mbalimbali baina yetu na kudumisha haki za binadamu na usawa wa kijamii.

Kutetea na kudumisha haki za binadamu na usawa wa kijamii ndilo lengo na msukumo wa kuwapo kwa stadihaki jamii. Taaluma ya stadihaki jamii hutambua kuwa haki za binadamu zinatakiwa kuwapo sanjari na uwajibikaji wa pamoja. Wazo la uwajibikaji wa pamoja huonesha ukweli kwamba haki za mtu binafsi zinaweza tu kupatikana siku hadi siku, kama watu watawajibika kwao wenyewe na katika mazingira yao, na umuhimu wa kujenga uhusiano kuelekea pande zote ndani ya jamii.

Kwa hiyo lengo kuu la stadihaki jamii ni kutetea haki za watu katika ngazi zote, na kurahisisha matokeo ambapo watu huwajibika kwa ajili ya ustawi wa kila mtu, kutambua na kuheshimu hali ya kutegemeana miongoni mwa watu na kati ya watu na mazingira.

Stadihaki jamii hujumuisha haki za kizazi cha kwanza, cha pili na cha tatu. Haki za kizazi cha kwanza zinahusu haki za kiraia na za kisiasa kama vile uhuru na dhamira ya kujieleza, uhuru kutoka kwenye mateso na vikwazo holela. Haki za kizazi cha pili ni zile za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni, ikiwa ni pamoja na haki ya kupata viwango stahiki vya elimu, huduma za afya, na makazi na haki ya lugha za wachache. Na haki za kizazi cha tatu zimelenga kwenye ulimwengu wa asili na haki ya viumbe hai na usawa wa vizazi vijavyo. Haki hizi hutegemea pande mbili kujiimarisha na huhusisha haki za kiumbe mmoja mmoja na pia haki za pamoja.

Katika mazingira fulani, "kutowadhuru wengine", na "kuheshimu tofauti mbalimbaii baina yetu" hunaweza kuleta migigoro na kutotangamana kwa maadili. Kwa mfano, kwa kisingizio cha utamaduni, haki mbalimbali, zikiwamo haki ya kuishi, haki za vikundi vya watu wachache kama vile wanawake na pia haki za wafanyao mapenzi ya jinsia moja, hukiukwa.  Viwango vya Kimataifa vya Elimu na Mafunzo ya Huduma Jamii hujishughulisha na suala hili changamani kwa kueleza kwamba wahudumu jamii huongozwa na mkabala wa haki za msingi za binadamu, wenye ufafanuzi unaosomeka hivi:

> "Mkabala huo unaweza kusaidia kuwapo kwa jitihada za kuwezesha mazungumzo ili kujenga maelewanopindi itokeapo kwamba baadhi ya imani za kitamaduni, maadili na mila zinakiuka haki za msingi za binadamu.  Kwa kuwa utamaduni hujengwa na jamii na pia hubadilika, basi kuna uwezekano wa kujengwa upya na kubadilika. Maelewano hayo, kujengwa upya, na kubadilika kwa utamaduni huweza kuimarishwa kwa njia ya kusikiliza, na kuelewa maadili, imani na mila ya jamii husika na pia kwa njia ya majadiliano ya kina na wahusika wa kundi husika la kitamaduni dhidi ya masuala mapana ya haki za binadamu".

**MAARIFA**

Stadihaki jamii huhusisha nyanja mbalimbali na huchunguza kwa upana nadharia na tafiti za kisayansi. 'Sayansi' katika muktadha huu hueleweka kwa maana yake ya msingi zaidi kama 'maarifa'. Stadihaki jamii huegemea katika misingi yake ya kinadharia na kitafiti ambayo inaendelea kuimarika, pamoja na nadharia kutoka sayansi nyingine za binadamu ikiwa ni pamoja na maendeleo ya jamii, mbinu za ufundishaji jamii, utawala, anthropolojia, ikolojia, uchumi, elimu, usimamizi, uuguzi, taaluma ya magonjwa ya akili, saikolojia, afya ya jamii na sosiolojia, japo haiishii katika nyanja hizo pekee. Upekee wa tafiti na nadharia za stadihaki jamii ni kwamba zenyewe ni tumizi na za kiukombozi. Tafiti na nadharia nyinigi za stadihaki jamii hujengwa kwa pamoja na watumiaji kwa maathiriano na njia ya majadiliano na hivyo, hutokana na mazingira halisi na mahususi ya kiutendaji.

Fasiri hii inatambua kwamba stadihaki jamii haitokani tu na mazingira mahususi ya kiutendaji na nadharia za kimagharibi, bali pia na maarifa ya wenyeji. Sehemu ya mtazamo wa kikoloni ni kwamba maarifa na nadharia za kimagharibi zimekumbatiwa sana na maarifa ya wenyeji yameshushwa thamani, hayahesabiki na huamuliwa na maarifa ya nadharia za kimagharibi. Fasiri hii mpya imejaribu kukomesha na kubadili mwelekeo huo kwa kutambua kwamba wenyeji wa kila mkoa/kanda, nchi au eneo wana maadili yao, namna za kujua na kuhamisha maarifa yao na wametoa michango mikubwa kwenye sayansi. Stadihaki jamii inataka kurekebisha ukoloni wa kisayansi za kimagharibi uliojengeka kihistoria na mamlaka ya kikoloni kwa kusikiliza na kujifunza kutoka kwa wenyeji ulimwenguni kote. Katika hali hii maarifa ya huduma jamii yataundwa kwa ushirikiano na kufahamika na wenyeji na kutekelezwa kwa usahihi zaidi, sio tu katika mazingira ya nyumbani bali pia ya kimataifa. Kutokana na kazi za Umoja wa Mataifa, Shirika la Kimataifa la stadihaki Jamii limefasili, wenyeji kama ifuatavyo:

1. Wale wanaoishi kwenye (au wanaendelea kujihusisha na) maeneo ya mababu yaliyo tofauti kijiogrogia.
2. Wanaoendeleza asasi tofauti za kijamii, kiuchumi, na kisiasa katika maeneo yao.
3. Wanaopenda kuendelea zaidi kuwa tofauti kiutamaduni, kijiografia na kiasasi kuliko kuchangamana pamoja kama taifa.
4. Wanaojitambulisha na kujibainisha kwa misingi ya uenyeji au ukabila.
   http://ifsw.org/policies/indigeneous-peoples

**UTENDAJI**

Uhalali na mamlaka ya stadihaki jamii huegemea katika kujipenyeza kwake pale ambapo watu hutagusana na mazingira yao. Mazingira hujumuisha mifumo tofauti ya kijamii ambamo watu hujumuishwa na mazingira asilia ya kijiografia amabayo yana athari kubwa katika maisha ya watu. Mbinu shirikishi inayotetewa katika stadihaki jamii huakisiwa katika dondoo hii: “Huhusisha watu na miundo kushugulikia changamoto za maisha ili kujenga ustawi.” Kadiri iwezekanavyo, stadihaki jamii hutetea kufanya kazi na watu zaidi kuliko kufanya kazi kwa ajili ya watu. Kufuatana na kielelezo cha maendeleo ya jamii, wastadihaki jamii hutumia maarifa mbalimbali, mbinu, mikakati, kanuni na shughuli kadha katika ngazi mbalimbali za mfumo zinazolenga kuuduimisha mifumo na/au jitihada za kuubadilisha. Utendaji wa stadihaki jamii huchukua shughuli nyingi zinazojumuisha tiba na ushauri wa aina mbalimbali, kazi za vikundi, na kazi za kijamii; kuunda na kuchambua sera; pamoja na utetezi na ushauri wa kisiasa. Kutokana na mtazamo wa kiukombozi, fasiri hii inaunga mkono kwamba mikakakti ya huduma jamii ilenge kuongeza matumaini ya watu, kujiamini, uwezo wa kiubunifu wa kukabili na kukosoa mfumo kandamizi, vyanzo vya dhuluma na vyanzo vya kimuundo vya ukiukwaji wa haki, hivyo kuweka vipengele vidogo na vikubwa pamoja ili kuunda kitu kikubwa cha pamoja, na mwelekeo binafsi kisiasa katika kushughulikia mambo. Malengo ya jumla ya stadihaki jamii ni ya kilimwengu lakini vipaumbele vyake kiutendaji vitatofuatiana kati ya nchi moja na nyingine, kutoka kipindi kimoja na kingine kutegemea hali ya kihistoria, kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Ni wajibu wa wastadihaki jamii duniani kote kutetea, kustawisha, na kutambua miiko na kanuni zilizoakisiwa kwenye fasiri hii. Fasiri ya stadihaki jamii inaweza kuwa na maana endapo tu wastadihaki jamii watajizatiti kutekeleza na kufanikisha maadili na matarajio yake.